

20. WE

20. WE

Karibu kwenye muhtasari wa kitabu cha ISHIRINI kwenye orodha ya vitabu 100 ninavyosoma kwa siku 100.

WE ni riwaya iliyoandikwa na Yevgeny Zamyatin inayohusu jamii ya binadamu miaka elfu moja ijayo, ambapo teknolojia imekuwa kubwa, udhibiti wa serikali ni mkubwa, ila bado watu wanabaki kuwa watu.



Tangazo linatolewa kwenye gazeti la serikali kwamba ndani ya siku 120 zijazo taifa la Marekani litakuwa limekamilisha chombo bora cha kwenda angani.

Chombo hicho kitaenda anga zima na kueleza ukuu wa Marekani kwa viumbe wa sayari nyingine ambao bado wako nyuma kimaendeleo.

Wito unatolewa kwa wanaoweza kufanya utunzi mbalimbali wa kulisifia taifa hilo, uwe ni nyimbo, mashairi na kadhalika ambavyo vitaenda na chombo hicho.

D-503 ambaye ni mtengenezaji wa chombo hicho anaelezea jinsi ambavyo kila kitu kwenye taifa hilo ni cha pamoja na siyo cha mtu binafsi.

Anaeleza kuwa yuko tayari kuripoti kila kitu kuhusu maisha ya zama hizo.

Matukio haya ni miaka elfu moja ijayo kutoka wakati wa kitabu kuandikwa (karne ya 20).

Katika kipindi hicho kila kitu kimepewa namba, mpaka watu wanajulikana kwa namba.

Na watu wote wanawaza kitu kimoja, hivyo kila mtu anajua mwingine anawaza nini.

Pia majengo yote yamejengwa kwa vioo mpaka barabara wanazotumia na mji umezungukwa na ukuta wa vioo ukitenganisha na maeneo mengine.



D-503 anatafakari na kuyaangalia mandhari na hali ya hewa. Anakumbuka watu wa zamani (sisi) walikuwa wakiandika sana mashairi na tungo mbalimbali kuhusu uzuri wa asili. Anashindwa kuelewa uzuri huo ni upi.

Anajiuliza kwa nini watu huwa wanaona uzuri kwenye kucheza mziki. Anajipa jibu kwamba ni kwa sababu uchezaji mziki ni kitendo kisichokuwa huru na kwa kuwa asili ya binadamu ni kutokuwa huru, huwa wanaona uzuri kwenye hilo.

Amakatishwa na O-90 ambaye ni mpenzi wake, amemfuata wawe na matembezi.

Wanatoka pamoja, barabarani wanakutana watu mbalimbali, kila mmoja ana namba yake.

Wanakutana na mwanamke ambaye anamsemesha, namba yake ni I-330, wanajadiliana mambo mbalimbali na wanapoachana mwanamke huyo anamtaka amyembelee baada ya kesho.

D-503 anaagana na mpenzi wake kwa kumbusu mara tatu na hapo wote wanajua baada ya siku inayofuata ndiyo siku yao ya kufanya mapenzi.



D-503 anaeleza kwamba jamii ya kipindi chao imetofautiana sana jamii za nyuma.

Kwanza kabisa hakuna aina yoyote ile ya usafiri na hakuna haja ya kufanya hivyo. Vita ya miaka 200 iliharibu barabara zote na zilipokuwa barabara kumeota majani na hivyo kuitwa ukuta wa kijani.

Pili kuna jedwali la matumizi ya muda, ambalo kila mtu anafundishwa tangu akiwa mtoto. Jendwali hilo lina matumizi ya muda wote wa siku nzima, yaani masaa 24 ya siku.

Watu wote wanaamka kwa muda mmoja, wanaenda kazini kwa muda mmoja, wanapumzika kwa muda mmoja, wanaanza kula na kumaliza kwa muda mmoja, wanaenda matembezi barabarani kwa muda mmoja na wanaenda kulala kwa muda mmoja. Yote hayo yanafanyika kwa kengele kugongwa kwenye muda fulani na hapo watu wanajua nini kinapaswa kufanyika.

D-503 anashangaa kwamba akisoma historia anaona jamii za nyuma kila mtu alikuwa anatumia muda wake anavyopanga mwenyewe, anashangaa hilo liliwezekanaje, maana ni vigumu kwa taifa kuwadhibiti watu kama wapo huru kutumia muda wao watakavyo.

Kitu cha tatu ni muda binafsi, mara mbili kila siku, saa 10 mpaka 11 jioni na saa 3 mpaka 4 usiku ni muda binafsi. Huo ndiyo muda pekee ambao mtu anapata wa kuwa mwenyewe kwenye siku yake, muda ambao hawanyi kile wanachofanya wengine. Ni katika muda huo tu ndiyo mtu ana uhuru wa kutumia muda wake atakavyo.

Muda mwingine wote wa siku kila ambacho mtu anafanya kinaonekana na wengine, hata kuoga. Nyumba zao zinejengwa kwa vioo na hivyo kila mtu anaona kila anachofanya mwingine. Katika muda binafsi mapazia yanaziba nyumba za watu na hapo ndipo wanakuwa na muda binafsi.

Kitu cha nne ni kufanya mapenzi na kuzaliana, D-503 anashangaa kwamba jamii za nyuma watu walikuwa wanaachwa wafanye mapenzi watakavyo na kuzaliana hovyoy. Katika jamii zao ufanyaji wa mapenzi unadhibitiwa na kupangwa na serikali na watu hawazaliani hovyoy.

Kwa kuwa bado kuna wachache wanapenda kurudi kwenye uhuru waliokuwa nao watu wa nyuma, serikali ina kitengo cha malezi ambapo kuna watu kazi yao ni kurekebisha wale ambao hawaendi sawa na utaratibu uliowekwa.

Kila kitu kinakokotolewa na kupangiliwa kwa namba ili serikali iweze kuwa na udhibiti mkubwa wa kila kitu.

Kitu pekee ambacho serikali haijaweza kutatua ni furaha na ndiyo maana imeweka muda wa kila mtu kuwa binafsi. Maana licha ya kila kitu kudhibitiwa na serikali, bado haijaweza kudhibiti furaha.

👉4

Siku hii D-503 amepangiwa kuwa kwenye ukumbi wa mikutano, kumbuka kila anachofanya mtu anakuwa amepangiwa.

Lakini pia ndiyo siku yake ya kufanya mapenzi na O-90 kwenye muda binafsi.

Anafika kwenye ukumbi, anakuja mtu kutoa mhadhara ambapo anaeleza jinsi watu wa zamani walivyokuwa wanafanya mambo wasiyoelewa.

Mhadhiri huyo anaeleza mfano wa mtu aliyeokota kipima mvua na kugundua mshale ukisimama kwenye mvua basi mvua inanyesha. Mtu huyo kwa kutaka sana mvua, analazimisha mshale uende kwenye mvua kwa kutoa zebaki kwenye kifaa hicho, lakini anashangaa mvua hainyeshi. Watu wanacheka sana na anawataka wasicheke, kwani bado hata kwenye zama zao watu wanafanya makosa ya aina hiyo.

Kinatambulishwa kifaa kipya cha muziki ambacho kinamwezesha mtu yeyote kutengeneza mziki mzuri ndani ya muda mfupi. Hii ni teknolojia kubwa ambayo watu wa zamani hawakuwa nayo.

Anamuona I-330 akipanda jukwaani na kuimba mziki mzuri, amevaa vizuri na kupendeza. Wote waliohudhuria hapo wanacheka na kufurahi sana.

Muda wa kuwa hapo unaisha, watu wanatawanyika, D-503 anarudi nyumbani na kukutana na O-90 ambapo wanafanya mapenzi kisha wanakuwa na maongezi ambapo wanajadiliana namba mbalimbali.

Wakati wa kufanya mapenzi wanakuwa na kibali cha kutumia mapazia. Muda mwingine wote wanakuwa wazi na hivyo kila wanachofanya kinaonekana.

D-503 anajiambia watu wa zamani walifanya maovu mengi kwa kuwa walikuwa na kuta za kujificha, katika kipindi chao, hakuna pa kujificha hivyo ni vigumu kufanya uovu wowote.

👉5

D-503 anaeleza kwamba kuna nguvu kuu mbili zinazotawala dunia; NJAA na MAPENZI.

Marekani kwa kujua hilo, ilihakikisha inazidhibiti nguvu hizo mbili kwa gharama kubwa.

Kwa upande wa njaa, ilihakikisha kunakuwa na kanuni sahihi ya mahesabu ya kupatikana kwa chakula kinachowatosha watu wote, hivyo hakuna tena tatizo la njaa.

Kwa upande wa mapenzi nako hesabu zilitumika kuleta usawa, maana watu wa zamani walikuwa wanachukiana na kuuana kwa sababu ya mapenzi.

Kuondoa hilo, serikali ilianzisha sheria ya mapenzi ambapo mtu anaomba na kupewa leseni ya kumtumia mtu mwingine kimapenzi.

Katika maombi hayo, watu wanafanyiwa kipimo cha homoni za mapenzi na kisha jendwali limaandaliwa la siku zipi wafanye mapenzi.

Kwa kutumia kanuni hiyo ya namba, tatizo la mapenzi linakuwa limetatuliwa na hakuna tena wivu baina ya watu.

D-503 anaeleza jinsi ilivyo vigumu kwake kuandika haya kwa sababu waandishi wamekuwa wanaandika kwa wasomaji waliopo au wajao, lakini siyo kuandika kwa wasomaji waliopita.

Vitu vingi ambavyo katika zama zao ni kawaida, ni vigumu kumwelezea mtu wa nyuma na akaelewa.



6

Saa kumi kasoro D-503 anapokea simu ya I-330 ambaye anamuuliza kama wanaweza kukutana kwenye muda binafsi ambao ni saa 10 mpaka 11. Anamjibu ndiyo, anamtaka wakutane kwenye nyumba ya kale.

Nje wanakutana na bibi mzee amekaa, wanamsalimia na kuingia ndani. Ndani ya nyumba hiyo kuna makumbusho mbalimbali ya watu wa kale, jinsi walivyoishi maisha yao.

D-503 anaeleza jinsi walivyokuwa wanahangaika na mambo yasiyo na tija.

Wanajadiliana mengi na anatambua wazi kwamba I-330 anamtaka kimapenzi, kwani kila anachofanya kinaashiria hivyo.

Saa 11 kasoro inafika, D-503 anasema inabidi aondoke, I-330 anamwambia wabaki pamoja hapo. D-503 anamwambia saa 11 anatakiwa kuripoti kwenye ukumbi wa mafunzo, I-330 anamwambia ana mwanaume ambaye ameandikishwa kwake kimapenzi ambaye ni daktari, anaweza kuongea naye amwandalie cheti kinachoonesha kwamba anaumwa.

D-503 hata akifanya hivyo, bado anatakiwa kutoa ripoti kwenye ofisi ya malezi, I-330 anampigia simu mtu mwingine na kumwacha D-503 aende zake.

Saa 11 kamili D- yupo kwenye ukumbi wa mafunzo na baadaye anarudi nyumbani akiwa amechoka sana hawezi hata kutoa ripoti kwenye ofisi ya malezi.



7

Usiku D-503 anaota ndoto ya vitu alivyoona kwenye nyumba ya kale. Hajawahi kuwa na ndoto kwenye maisha yake. Kwenye zama zao, ndoto ni dalili ya ugonjwa wa akili. Lakini anakumbuka vitu alivyoota ni vile alivyoona kwenye nyumba ya kale.

Saa moja inafika, muda wa kila mtu kuamka, anaamka kama wengine, anapata kifungua kinywa na kuelekea kazini.

Anakutana na S-4711 ambaye wanafanya kazi pamoja na anamueleza kwamba jana alienda kwenye nyumba ya kale, anampongeza kwa hilo. Anaendelea kumweleza kwamba hakuwa peke yake, aliongozana na I-330, S-4711 anamwambia ana bahati sana, maana huyo ni mwanamke ambaye wengi wanamkubali sana.

Anashangazwa na hilo, lakini hataki kuonesha mshangao wake, hivyo anaficha uso wake kwa kusoma gazeti. Kwenye gazeti hilo anasoma habari kwamba kuna kikundi kinegundulika ambacho kinaonekana kupambana kupata uhuru kutoka kwenye taifa.

Habari hiyo inamkasirisha D-503 ambaye anasema uhuru ndiyo chanzo cha maovu yote. Pale mtu anapokuwa huru kufanya chochote anachotaka, ndipo anapofanya maovu. Anajiambia kama mtu hana uhuru kabisa, hawezi kufanya uhalifu wowote. Hivyo kufuta uhalifu kabisa itafikiwa kwa kufuta uhuru kabisa.

D-503 anajiambia inabidi aende kwenye ofisi ya malezi akaeleze alipokuwa jana.

Saa kumi anatoka kazini na kupanga kwenda moja kwa moja ofisi ya malezi, lakini njiani anakutana na O-90 ambaye anamuuliza kama anaenda matembezini, anajibu hapana.

D-503 anamwambia anaenda ofisi ya malezi, O- anashangazwa nini kinampeleka huko. D-anajibu kwa ukali, kitu kinachomfanya O- aone hayuko sawa, hivyo anamshauri aende hospitali.

D-503 anakubali kwenda hospitali maana akikumbuka na ndoto ya jana anaona wazi hayuko sawa.

Huko anachelewa kurudi na kushindwa kwenda ofisi ya malezi.
Anarudi nyumbani na kulala.

👉8

D-503 anakumbuka wakati wako shule, siku wanafundiasha kipeo cha hasi moja, anakumbuka jinsi alivyokataa uwepo wa namba hiyo.

Mawazo hayo yamemjia tena na anatamani sana kuyafuta kwenye akili yake.

Yuko nje ya jengo la ofisi za malezi, anatamani sana kuingia lakini ndani yake kuna kitu kinamzuia.

Akiwa pale rafiki yake waliyesoma naye anayeitwa R-13 anakuja akiwa ameambatana na O-90.

Rafiki yake huyo ni mshairi, anamuuliza D-503 anaonekana kuwa na mawazo, kuna hesabu zinamsumbua?

D-503 anamjibu hapana, anataka tu muda wa kuwa peke yake. Anawataka waongozane, ila O- anamwambia leo ni zamu ya R-13. Wote wawili wamepangiwa kumtumia O-90 kimapenzi na hilo limefanya urafiki wao kuwa karibu zaidi.

D-503 anawasindikiza mpaka kwa R-13 wanakumbushana wakati wa shule na R- anamuuliza amefikia wapi kwenye kukamilisha chombo cha angani, maana wao washairi wanazidi kuandika na kama chombo kitachelewa watajikuta wana mzigo mkubwa wa kwenda nao.

D-503 anaangalia saa, ni saa 10 na dakika 25, anaona anachukua muda wao mwingi, zimebaki dakika 35 tu za muda binafsi, hivyo anatoka na kuwaacha.

👉9

D-503 anaeleza kwamba wamehudhuria ibada na dini ya kipindi hicho ni tofauti na kipindi cha sasa. Dini inadhibitiwa na serikali na mungu wao siyo kama wa watu wa zamani, ni mungu wanayemuona na ambaye matakwa yake yanajulikana.

Mungu wao anaitwa Well-Doer (mtenda mema) ambaye ndiye mkuu wa kutengo cha malezi. Yeye ndiye huwa anatoa adhabu kwa wote wanaofanya uhalifu.

Katika siku hii mhalifu mmoja anapewa adhabu ya kifo, kabla ya adhabu hiyo R-13 anapanda jukwaani na kuimba shauri la kifo.

Kisha mhalifu anaenda kwenye mashine ya kifo na Well-Doer anaiwasha mashine hiyo. Umati unashuhudia jinsi mashine hiyo inavyoyeyusha mwili wake na kuwa maji.

Mwisho wanawake wanampelekea maua Well-Doer, D-503 anajiambia haoni uzuri wowote kwenye maua kama wengine wanavyoona. Yeye anaona uzuri kwenye vitu vyenye matumizi kama mashine, kanuni za hisabati, chakula n.k.

👉10

Akiwa kazini D-503 anapokea barua inayomweleza kwamba anawajibika kimapenzi kwa I-330 na siku hiyo saa tatu usiku anapaswa kuwa kwake.

Anashangazwa na hilo, hakulitegemea hasa baada ya kumkatalia walipokutana mara ya mwisho.

Anajiuliza O-90 atachukuliaje hilo, huenda ataona walipanga, wakati yeye hakujua lolote.

Saa tatu anafika kwa I-330 anamsifia kwa kuwahi, anamwambia alijua asingeweza kwenda kuripoti tukio la siku ile kwenye ofisi ya maadili. Na sasa inabidi amsikilize maana ana kosa la kutokuripoti, akienda kumripoti yeye, ataadhibiwa vibaya.

I-330 anashusha mapazia na kisha wanafanya mapenzi. Baada ya kumaliza I-330 anaanza kuvuta sigara na kunywa pombe, D-503 anashangazwa na hilo, anamwambia anajua kabisa ni kosa kisheria kwa mtu yeyote kutumia kilevi cha aina yoyote. Adhabu yake ni kifo, maana bora taifa lipoteze watu wachache kwa adhabu kuliko kupoteza wengi kwa madhara ya ulevi.

I-330 anamwambia anajua hawezi kwenda kuripoti, anamshawishi naye pia anywe. D-503 anashawishika na kunywa na baada ya kunywa anaona mabadiliko makubwa ndani yake. Anajiona ana nafsi mbili, ya zamani na ya sasa.

Anakuuliza I-330 amepata wapi pombe hiyo, anamjibu daktari ambaye ni mpenzi wake amempa. D-503 anajibu kwa hasira hataki kusikia ana mpenzi mwingine, yeye ni wake tu.

Anamvuta ili wafanye tena mapenzi, anamuonesha saa, ni saa 4 na dakika 20 usiku, D-503 anapatwa

na taharuki, saa 4 na dakika 30 anapaswa kuwa nyumbani kwake.

Pombe zinakatika ghafla, anatoka haraka na kukimbia nyumbani, kasoro dakika moja anafika.

Anajaribu kulala lakini usingizi hauji, mawazo mengi yanamjia na anaona jinsi anavyomchukia I-330.

Anajikumbusha kwamba ni sheria kila mtu kulala usiku kama ilivyo kufanya kazi mchana. Na mtu asiyelala usiku anatenda kosa ambalo adhabu yake ni kubwa. Pamoja na kujikumbusha hivi, bado hapati usingizi.

👉11

D-503 anaamka akiwa amechoka na bado anaona ndani yake kuna nafsi mbili. Nafsi ya zamani ambayo ndiyo halisi na nafsi mpya ambayo siyo halisi. Anakumbuka yaliyotokea jana na hajui kilichomfanya afikie hivyo ni kufanya mapenzi na I-330 au kunywa pombe.

R-13 anakuja kwake D-503 hataki kuonesha ana tatizo lolote, anamsifia R- kwa shairi lake la siku ya hukumu. R- anamwambia amechoshwa na adhabu hizo za kifo na hali ya kukosa uhuru. Anamweleza kwamba watu wa zamani walipewa kuchagua kati ya uhuru bila furaha au furaha bila uhuru, wao wakachagua uhuru na wakawa huru kuishi watakavyo, ila hawakuwa na furaha. Lakini kwa zama zao, wameweza kubadili hilo, wameondoa uhuru kabisa ili kupata furaha, kitu ambacho kimefanya maisha yawe rahisi kama ya watoto wadogo.

R-13 anamwezela D-503 kwamba anaendelea kuandika mashairi kwa ajili ya chombo chake.

Anamuuliza kwa siku ambazo O-90 amepangiwa kwake atakuwepo au ataenda kwa mwingine kama siku iliyopita? D-503 anajibu atakuwepo. R- anamuuliza kwa miaka mingi wamekuwa wao watatu, sasa ameongezeka wa nne, ni nani?

D-503 anamuuliza kama amewahi kuonja pombe au sigara. R- anamjibu hajawahi, ila anasikia kuna mwanamke, kabla hajamalizia D- anamwambia I-330, R- anamwambia kumbe na wewe tayari?

D-503 anashikwa na hasira, anamuuliza tayari nini, anamtaka amweleze, lakini R-13 anamwambia kilichomleta hapo ni kumpa kitabu chake kipya, anampa na kuondoka.

D-503 anabaki akiwa na hasira, anajiuliza kumbe kitu kilichokuwa kinaitwa wivu kwa watu wa zamani kipo. Anajiambia labda aende kwa R- waongee, lakini anajiambia hataenda na kuanzia sasa hataki tena urafiki naye.

👉12

D-503 anajiaminisha kwamba ataendelea vizuri. Ameanza kupata usingizi japo hali ya nafsi mbili haijaondoka.

Anapanda treni huku akisoma kitabu cha ushauri cha R-13, anahisu nyuma yake kuna mtu anamwangalia, hageuki kumwangalia ila anahisi ni R-13.

Anasona shairi kuhusu furaha, jinsi kanuni ya kihesabu ya furaha ilivyo kama hesabu ya mbili mara mbili ni nne.

Anaendelea kutafakari maisha ya watu wa zamani na maisha ya zama zake. Jinsi washairi wa zamani walivyokuwa wachache na walivyojificha. Lakini kwenye zama zao ushairi umefanywa kuwa taasisi ya serikali. Kadhalika kwa mungu wa zamani alikuwa amejificha, ila mungu wao wanamuona moja kwa moja.

Anaona hatua ambazi kizazi chao kimepiga ambazo kwa kizazi cha zamani zilikuwa ndoto tu.

👉13

D-503 anaamka akiwa anajisikia vizuri, hiyo ni siku ya O-90 kuja mwake wafanye mapenzi.

Anaenda kazini na saa sita kasoro anarudi nyumbani mara moja kabla shifti ya saa 6 haijaanza. Simu inaita na sauti inamwambia imeshukuru yupo nyumbani, wakutane kwenye kona saa sita kamili.

D-503 anamjibu anajua kabisa kwamba saa 6 anatakiwa kuwa kazini. Sauti inamwambia anajua kabisa anapaswa kufanya anachomwambia.

D-503 anaona hana namna, anaenda kumsubiri I-330 kwenye kona, ambaye anachelewa kufika.

Anapofika anamwambia kwa sasa tayari ameshachelewa kazini. Anamkumbatia na D-503 anasahau wasiwasi wote aliokuwa nao kuhusu kazi.

I- anamwambia waongozane, wanaenda mpaka hospitali, wanapokelewa na daktari, I- anaongea naye

na kisha wote wawili wanapewa vyeti kwamba wanaumwa na hivyo hawawezi kuhudhuria kazini. D-503 anajiona anekuwa mwizi wa taifa lake, ameliibia taifa muda wa kazi, lakini anapojiona yuko na I-330 yote hayo anayasahau.

Wanaondoka na kuelekea nyumba ya kale, wanaingia ndani na D- anaona vyote alivyoviota siku aliyotoka pale. Anapata tamaa kubwa ya kufanya mapenzi na I- lakini wakati anajiandaa, I- anatoweka. Anaangalia mlango umefungwa kama ulivyokuwa na hakuna mlango mwingine kwenye chumba hicho.

Anashindwa kuelewa hilo limetokeaje, anaona kama yupo ndotoni lakini anagundua ni uhalisia.

👉14

D-503 anarudi nyumbani na kumsubiri O-90 kwa kuwa ndiyo siku yao.

Anaenda kwa mdhibiti wa jengo kuomba kibali cha kushusha mapazia, anamwambia leo hayuko sawa. D-503 anamjibu anaumwa na kumwonesha cheti cha daktari.

Anarudi chumbani kwake na kumsubiri O- ambaye anafika saa tatu na nusu.

O-90 anamlalamikia kwamba kwa sasa amebadilika sana na siyo wake tena, kila anapomtafuta hampati.

D-503 anafikiria hajawahi kujiona yeye ni wa mtu, labda kwa sasa. Anamwambia O- kwamba bado hajisikii vizuri, ameenda kwa daktari tena na anaamini atakaa sawa.

O-90 analala kitandani akilia, D-503 amekaa chini akitafakari kuhusu hali anayopitia sasa.

O- ananyanyuka na kuondoka kwa hasira, akimwambia D- asimfuata tena.

D-503 anabaki akifikiria jinsi ambavyo I-330 amepelekea kumpoteza rafiki yake R-13 na sasa mpenzi wake O-90.

Anajiuliza hajui atakaporudi kipi kingine kitabadilika kwenye maisha yake.

👉15

D-503 anaenda kazini na kila mtu anamuulizia kwa nini hakuwepo jana.

Anaambiwa kazi nyingi zimesimama kwa kuwa hakuwepo na pia kuna ajali ilitokea, mtu asiye na namba alikuwa ameingia kwenye chombo cha kwenda angani, aliweza kutolewa na uchunguzi unaendelea.

Mtu mwingine anamuuliza unaendeleaje? Anauliza kuendeleaje vipi? Na hapo anashtuka, amesahau hakuwa kazini jana na amedanganya.

Hilo linamfanya ajione yuko njia panda, kuanzia sasa maisha yake hayatakuwa rahisi tena, maana mtu ulishadanganya inabidi kila wakati uwe na kumbukumbu ili kulinda uongo wako.

Anaona atakuwa na maisha ya mateso.

Akiwa anafikiria hayo mfanyakazi mwingine anamuuliza ana shida gani, mbona anamuita kwa muda mrefu haitiki?

Hapo D- anajiona anazidisha matatizo yake, lakini pamoja na hayo bado anamfikiria sana I-330.

👉16

Tangu I-330 atoweke hawajaonana, kila mara anamfikiria na kuona hawezi kuishi bila yeye.

Anapokea cheti kwamba I- atakuja kwake, anamsubiri lakini haji.

Siku moja anaamua kwenda kukaa nje ya jengo analokaa I- muda wote wa saa binafsi hamuoni.

Bado hajisikii vizuri, anatamani sana amuone I- na kumweleza hawezi kuishi bila yeye.

Akiwa hapo anajiuliza afanye nini, anafikiria aende kwa daktari ila anapata uzito.

Ghafla S- anajitokeza na kumwambia waongozane kwenye kwa daktari. Baada ya kumweleza daktari yanayomsumbua, anamwambia ameingiliwa na roho.

D-503 haamini, mambo ya kuingiliwa na roho ni ya zama zilizopita, kwenye zama zao hilo halipo.

Daktari anamwambia siyo yeye tu, kumekuwa na wimbi la watu kuingiliwa na roho.

Daktari anamwambia tiba pekee ni kufanyiwa upasuaji ili kuondoa kabisa roho iliyomuingia. Lakini wanashindwa kufanya upasuaji huo kwa kuwa D- ni mtengenezaji wa chombo cha kwenda angani na upasuaji huo unaweza kuathiri hilo.

Daktari anamwambia kwa sasa anaweza kuondokana na hali hiyo kwa kutembea kwa muda mrefu.

Anamwandikia cheti cha kutokwenda kazini kwa siku mbili na atumie muda huo kutembea sana.
D- anaondoka akiwa na matumaini makubwa.

👉17

D-503 anaanza matembezi yake kama alivyoshauriwa, anaangalia jinsi majengo na kuta zilivyojengwa, kitu ambacho ni maendeleo ya kizazi chao.

Anatafakari ni lini ugonjwa wake umemuanza na anakumbuka ni baada ya kuitembelea nyumba ya zamani, hivyo nyumba hiyo ndiyo chanzo cha matatizo yake.

Anaenda mpaka kwenye nyumba ya kale na kushawishika kuingia kuangalia kama I-330 yupo.

Mlangoni anakutana na mwanamke mzee wanayemkutaga hapo mara zote. Anamuuliza kama I- yupo hapo, anamjibu amefika muda si mrefu.

D- anaingia haraka na kwenda kwenye chumba walichokuwa mara ya mwisho, lakini hamkuti I-, anajaribu kuangalia vyumba vingine na kukuta vimefungwa. Anasikia sauti ya mtu anapita, kuangalia ni S-, wazo linamjia, isijekuwa S- ndiyo I-, anajiuliza hilo linawezekanaje?

Anajificha ili S- asimuone. Sehemu aliyojificha anajikuta anaingia kwenye hiza asilolielewa na kujikuta yuko kwenye chumba cha daktari, ambaye anamuuliza anafanya nini hapo, aondoke. Mara anamuona I- ambaye anakuja na kumshika, anamweleza jinsi madaktari walivyomwambia, anacheka sana.

I- anamwambia wakutane siku inayofuata baada ya kesho, saa kumi, kisha anaondoka.

D-503 anashindwa kuelewa kama hiyo ni ndoto au matukio yaliyotokea. Anajiambia atajua hiyo siku baada ya kesho.

👉18

D-503 analala usingizi mzito siku hiyo, lakini bado ndito hazimuishi. Anamuona I-330 akiwa kwenye kabati la nguo na kuingia kumkumbatia. Anapoamka hajui kama ni kitu kimetokea kweli au ni ndoto.

Anashangazwa jinsi ambavyo hata kazi yake ya mwanahisabati imeathiriwa sana na hali anayopitia.

Anaendelea na zoezi ambalo daktari amemshauri, la kufanya matembezi.

Muda anaofanya matembezi yuko peke yake, wengine wote wako kwenye majukumu yao kama ratiba zao zinavyoonesha. Anajiona kama kidole kilichotengwa na mwili.

Anapokea barua kutoka kwa O-90 ambaye anameambia kwa siku chache zilizopita maisha yake yamekuwa magumu sana, hawezi kuishi bila yeye, kwa sababu anampenda sana.

Lakini anatambua kwamba hiki ni kipindi ambacho D-503 anapaswa kuwa mwenyewe, hamhitaji mtu mwingine yeyote, hivyo kwa kuwa anampenda sana, atafanga lililo jema kwake kwa kumuacha.

Ataenda kufuta jina lake kwenye watu wanaomtumia kimapenzi, anajua hatakuwa na furaha tena lakini amefanya kilicho sahihi.

👉19

Siku ambayo I-330 alimuahidi wataonana imefika. D-503 anafanya kazi kwa hamasa kubwa, akisubiri muda ufike.

Saa 10 anarudi nyumbani, kila sauti ya mtu anamsikia akipita kwenye korido anafikiri ni yeye, lakini siyo.

Baadaye anakuja mtu na kumletea bahasha, inatoka kwa I- ina kadi ya kufanya mapenzi siku hiyo na ujumbe unaomwambia saa tatu ikifika ashushe mapazia kama yuko naye, anataka wajue yuko hapo.

Ujumbe huo unamchanganya sana D- hajui kwa nini anamfanyia hivyo, anataka sana waonane.

Anatamani angekuwa na mapumziko leo akatembee arudi amechoka na alale, ila anatakiwa kwenye kwenye ukumbi wa mihadhara.

Anaenda na baadaye kurudi nyumbani, anamkuta O-90 akimsubiri kwenye chumba chake, anamuuliza kama amepata barua yake, anajibu ndiyo. O- anamwambia basi atamuacha kama alivyoahidi, ila anataka ampe mimba kabla hawajaachana.

D-503 anamwambia anajua fika hiyo ni hatari, atahukumiwa kifo kama atabeba mimba. O- anamjibu hajali, anachotaka ni abebe mimba yake hata kwa muda mfupi tu.

D-503 anamjibu kama hicho ndiyo anataka basi atampatia, anaenda kubadili cheti cha kufanya mapenzi na wanafanya mapenzi.



20

D-503 anajiona akiwa na utulivu mkubwa sasa, hata roho iliyokuwa inamsumbua kwa sasa siyo kama awali.

Anajua muda wowote 0-90 atapoteza uhai wake na kama atabanwa na kumtaja basi na yeye pia atapoteza uhai wake.

Hilo linamfanya atafakari mengi, kwenye zama zao ambapo kanuni za hisabati ndiyo zinaamua kila kitu na sheria nne za kuumlisha, kutoa, kugawanya na kuzidisha ndiyo zinazotumika kufanya maamuzi.

Anaona jinsi vizazi vya kale vilivyokuwa vikitekeleza adhabu kwa wakosaji kwa kutumia njia mbalimbali ikiwepo mauaji ya kikatili.

Anaona japo adhabu ni zile zile, lakini katika zama zao zinatekelezwa kwa ustaarabu mzuri.



21

D-503 anaendelea kumsuburi I-330 lakini haji. Jana ilikuwa siku ya kuja kwake ila hakuja, alituma kadi na ujumbe.

D- anajiambia atakuwa na utulivu na kufanya kile anachomwambia, siyo kwa sababu hawezi kufanya kinyume, ila kwa kuwa anapata muda wa kuandika. Pale anaposhusha mapazia na kuwa mwenyewe, anapata utulivu mkubwa wa kuandika.

Pamoja na yote bado anamsubiri kwa hamu kubwa arudi.

Anaondoka kwenda kwenye nyumba ya kale, mwanamke mzee anayemkutaga pale anamwambia hakuna mtu, anasisitiza aingie. Anaingia na hakuna yeyote, akiwa anazunguka hapo S- anakuja, anamuuliza anaendeleaje, anajibu vizuri. Anampongeza na kumtaka awe mwangalifu.

Anarudi nyumbani kwake, mwanamke mzee ambaye huwa anamletea barua anakuja kwake, anamweleza jinsi amekuwa hamuoni akiwa sawa na kumwahidi kuwa tayari kumsaidia kwa kile anachopitia.

D-503 bado anaandamwa na ndoto zile asizozielewa na zisizoisha.



22

D-503 yuko kwenye matembezi na watu wengine na ghafla mbele yao anatokea mwanamke ambaye hana namba na anakimbia.

D- anahisi ni I- na kuanza kumkimbia, anapomkaribia anagundua siye.

Anatafuta njia ya kuwafanya wengine wasichukulie vibaya kile alichofanya, anataka aseme kwa sauti mkamateni huyo, ila kabla hajasema yeye anakuwa ameshakamatwa.

Anapelekwa mahali asipoelewa na anayewapokea anasema inaonekana D- hayupo sawa hivyo hawezi kudhibiti hisia zake. Anaandikiwa cheti na kuachiliwa.

Anarudi kwenye matembezi, huku akiendelea kumfikiria I-.



23

D-503 anapitia kwa mdhibiti wa jengo, mwanamke mzee anayempaga barua ambaye namba yake inaanza na U-.

U- anamwambia D- hali yake siyo nzuri na hakuna anayeonekana kumjali na kumsaidia kwenye hilo.

D-503 anakiri ni kweli anaumwa maana ameingiliwa na roho ambayo haiponyeki.

Anarudi chumbani na kumkuta I-330 anamsuburi, anaishiwa nguvu zote na kujikuta amekaa chini ya miguu yake, akimuuliza kwa nini amemuacha muda wote huo.

I- anamjibu alikuwa anampima ili aone kweli kama atafanya kila anachomwambia na kama ni wake tu, mtihani ambao amefaulu.

D-503 anamtaka I- amwelezee yote ambayo amepitia, kuanzia kwenye nyumba ya kale, korido ya giza aliyopita na hata ndoto zinazomjia.

I- anamwuliza kama yuko tayari kumfuata popote atakapompeleka, anajibu ndiyo. Anamwahidi atamuelezea hayo yote siku zijazo.

I- anaondoka na kumuacha pale.



24

Kesho ni siku ya sikukuu, siku ambayo watu wote wanakutana pamoja na kufanya uchaguzi wa Well-Doer.

D-503 anaelezea jinsi uchaguzi wa zama zao ulivyo wa tofauti, upigaji kuwa ni wa wazi na siyo siri kama zama zilizopita.

Kila mtu anajua nani kamchagua nani. Na matokeo yanajulikana mapema kabisa nani anashinda. Hivyo chaguzi za zama zao ni rahisi na hazina changamoto kama chaguzi za zama za nyuma.

D-503 anajiandaa kwa sherehe za kesho, anatamani sana angekuwa na I-330. Anamipigia simu kumwomba kesho wawe pamoja, I- anamjibu haitawezekana, na sababu ataiona mwenyewe kesho hiyo.



25

Siku ya sherehe imefika, watu wamekusanyika. D-503 anamuona S- na kukumbuka kwamba kuna kitu amekuwa hakielewi kati ya S- ma I-330 anajiambia siku moja ataelewa.

Baadaye anamuona I-330 akiwa ameongozana na R-13, roho inamuuma sana, anajiuliza kwa nini amemfanyia hivyo.

Wakati wa kupiga kura umefika, wanaulizwa wanaosema ndiyo wanyooshe mikono, D- ananyoosha mkono wake pamoja na wengine wengi.

Kisha wanaulizwa wanaopinga, hapa huwa haitegemewi kuwepo kwa wapingaji. Lakini safari hii kuna wengi wamenyoosha mkono kupinga na mmoja wao ni I-330.

Hali hiyo inaleta taharuki na R- anamtoa I- haraka kwenye eneo hilo.

D- anawafuata na kumchukua I- kutoka kwa R- na kwenda naye yeye.

I- anamwambia D- anaamini kesho itakuwa tofauti na kama hakutakuwa na changamoto yoyote atampeleka kule alikomuahidi.



26

D-503 anaaamka na kukumbuka kilichotokea siku iliyopita.

Ilikuwa siku ya sherehe ambapo Well-Doer yule yule amechaguliwa tena kwa kishindo kwa mara ya 48, kulitokes mtafaruku kidogo ambapo maadui wa furaha walitaka kuvuruga uchaguzi lakini hawakufanikiwa.

Kura zao za hapana hazikuhesabiwa kwa sababu kufanya hivyo kungewapa ushujaa.

Leo saa sita mchana kutakuwa na mkutano wa pamoja wa taasisi kubwa tatu; Utawala, Afya na Malezi.

Kunategemea kutolewa kwa amri mpya baada ya mkutano huo.

D-503 anatoka kwenda kazini na njiani anaona watu wakikwepa kona fulani, anafika hapo na kuona karatasi imebandikwa ukutani ba kuandikwa MEPHI.

Anamuona S- akikazana kuitos karatasi hiyo lakini haifikii. Huku wengine wakikwepa kumsaidia ili wasionekane wanahusika.

D- anakumbuka S- amekuwa anamsaidia mara kwa mara, hivyo na yeye anamsaidia kutoa karatasi hiyo.

Anaendelea kwenda na kugundua kila mahali karatasi hizo zimebandikwa.

Anafika kazini na kujadiliana na mwenzake kama wanaweza kuanza kukijaribu chombo cha angani.



27

D-503 anajikuta akiwa mwenyewe kwenye korido zenye giza. I-330 alimwambia watakutana hapo saa 10, ila muda umefika hamuoni. Anasubiri kwa dakika 10 baadaye na kuamua kuondoka.

Ghafla anasikia mlango umefunguliwa na I- anamsemesha. Wanaongozana na kwenda asipojua, anajikuta yuko eneo la tofauti, I- anamwambia wametoka nje ya kuta za taifa.

Wanakuta kundi kubwa la watu wamekaa chini ya mlima, watu hao wanafanana na watu wa zamani, hawana namba kama watu wa zama hizo.

I- anapanda juu na kuanza kuwahutubia. Anawaambi mipango yao ya kuvunja kuta inakwenda vizuri.

Na sasa mtengenezaji wa chombo cha angani yuko pamoja nao, hivyo kitakapokamilika wataenda nacho angani.

D-503 anajiona wa tofauti, anajiamini zaidi na kujiona ni wa juu kuliko alivyokuwa anajichukulia. Anamwambia I- amemuona mtu kama S- katikati ya watu hao. I- anamjibu hilo haliwezekani, hawezi kufika hapo walipo. Kwani wao wanahangaika kupambana nao ndani ya kuta. D-503 anashindwa kuelewa kama haya yanatokea kweli au yuko ndotoni.

👉28

D-503 anaelezea jinsi kufikiri kwake kumebadilika tangu ametoka nje ya ukuta, hakuwahi kufikiri kuna watu wa aina hiyo wanaoishi nje ya ukuta wa mji wao.

Akiwa ndani kwake, I-330 na U- wanakuja pamoja, I- anamuuliza D- kama amempa mwanamke huyo jukumu la kumlinda, maana amekuwa anamzuia asimuone.

U- anasema D- kwa hali yake ni kama mtoto, anapaswa kulindwa.

D- anamtaka U- aondoke mara moja na anamuomba I- msamaha kwa hilo. Anamwambia yuko tayari kwa lolote kwake, kwani tangu aliyoona siku ya jana, amegundua kuna mengi hajui.

D- anamtaka I- amwelezee kuhusu wale watu aliomuonesha jana. I- anamueleza ni waliosalia kwenye vita ya miaka 200 ambayo Marekani ilipigana na jamii nyingine na ikashinda kisha kujenga ukuta. Hao walibaki nje ya ukuta na kupambana kuyaendesha maisha yao na hilo limewawezesha kuwa imara kuliko walio ndani ya ukuta.

Anamweleza watu hao ni jamii ya Mephisto ambao kwa kifupi wanaitwa Mephi.

D- anamwambia wanachofanya ni hatari, kikundi kidogo cha watu kukabiliana na taifa kubwa ni kutafuta kujiua. I- anamwambia kwa sasa hawana muda mwingi, wanapaswa kuchukua hatua.

Wakiwa hapo mtu ambaye huwa anatumwa na I- kuleta ujumbe kwa D- anaingia na kusema kuna msako unapita chumba kwa chumba, unaongozwa na S.

I- na mtu huyo wanatoweka, D- anabaki akiwa na hofu kubwa. Watu wa msako wanaingia, wanaongozana na U- ambaye anawaambia huyu ni D- mtengenezaji wa chombo cha angani na muda mwingi hukaa hivyo na vitabu vyake akisoma au kuandika.

Wanaondoka na kumuacha, baadaye U- anamwambia amshukuru sana, maana kama siyo yeye, mambo yasingekuwa mazuri kwake.

Anasikia msakk huo umeondoka na watu watatu ambao hakuna anayejua wamepelekwa wapi na hakuna anayethubutu kuhoji.

👉29

I-330 amemwambia D- wakutane kwenye nyumba ya kale. Akiwa anaelekea huko anakutana na O-90 ambaye anaonekana kuwa na furaha.

Anamkaribia na kumwambia ana furaha sana kwa kiumbe aliye ndani yake. Japo anajua hatamuona au kumlea, lakini kuwa naye inatosha.

D-503 anamwambia huo siyo wakati wa kufurahia, kwani mimba yake inakua na siku siyo nyingi itagundulika na atauawa.

Lakini anamwambia anajua namna wanaweza kuepusha hilo. Anamweleza kuhusu I-330 na kwamba anaweza kuwasaidia kuepusha kifo.

O-90 anamwambia hawezi kukubali kusaidiwa na I- na amuache kwani hapaswi kujali chochote kuhusu yeye, anaondoka na kumuacha.

D-503 anaelekea kwenye nyumba ya kale.

👉30

I-330 anamwambia D- kwamba siku inayofuata baada ya kesho ndiyo siku imepangwa kujaribu chombo cha angani. Na hiyo ndiyo siku ambayo wanapaswa kukichukua chombo hicho.

D-503 anamwambia hajaelewa, I- anamfafanulia kwamba katika watu waliokamatwa siku ya jana, kuba ambao ni Mephi, hivyo hawana tena muda wa kusubiri.

Anamwambia siku hiyo saa sita mchana, kengele itakapogongwa na watu kwenda kula, yeye abaki ndani ambapo chombo kipo na awafungie wengine nje, kisha I- atakuja na waondoke na chombo.

Wakishakidhibiti chombo, hakuna atakayeweza kuwashambulia maana wakijaribu hivyo watalipua mji mzima.

D-503 anakataa na kusema hilo haliwezekani, hayo yatakuwa ni mapinduzi wakati Well-Doer alishasema vita ya miaka 200 ndiyo yalikuwa mapinduzi ya mwisho.

I- anamwambia wewe ni mwanahisabati, nitajie namba kubwa kuliko zote, namba ya mwisho kabisa kwa ukubwa. D-503 anajibu hakuna mwisho wa namba. Hapo I- anamjibu mapinduzi pia hayana mwisho, wamekuwa wanadanganywa tu.

D-503 anasema lakini ya nini kufanya hivyo wakati watu wanaishi vizuri na kwa furaha tu. I- anamwambia huo ni uongo mwingine ambao taifa limewalisha.

I- anamsisitiza akumbuke saa sita mchana kufanya alivyomwelekeza, D- anamwambia atakumbuka.

👉31

D-503 akiwa kwenye mawazo makubwa ya kile kinachokwenda kutokea, anapata taarifa njema zilizoandikwa kwenye gazeti la serikali.

Taarifa hizo zinasema imegundulika njia ya kuwawezesha watu kuwa na ukamilifu na hivyo kuwa na furaha kwa asilimia 100.

Chanzo cha watu kukosa furaha ni tamaa zao na tamaa hizo zinazalishwa na sehemu ya mbele ya ubongo.

Hivyo imegundulika tiba ya mionzi (x-ray) ambayo mtu akipewa kwenye paji la uso anaondokana kabisa na tamaa na kukosa ukamilifu.

D-503 anafurahishwa na habari hizo, anajua tatizo lake la kusumbuliwa ba ndoto linakwenda kupata tiba.

Anawasiliana I- kwamba waonane siku hiyo. Anatoka kwenda kazini na mfanyakazi mwenzake anamwambia majaribio ya chombo cha angani yameahirishwa kwa siku moja. D-503 anazidi kuona hizo ni habari njema.

Anaenda kuonana na I- ambaye ameshapata taarifa hizo pia. I- anamwambia ni wakati wa kuagana, D- anamuuliza kwa nini anajibu kwa tiba iliyopatikana, akishapewa hatakuwa tena na ugonjwa unaomfanya ampende na kumtaka yeye tu.

D- anajibu hataki kitu kingine kwenye maisha zaidi ya kuwa na I-.

I- anamwambia inabidi achague, kupewa mionzi na kuwa na furaha kwa asilimia 100 au kubaki na yeye. D- anamjibu anachagua kubaki na yeye.

Anamwambia basi wakutane kesho kama walivyopanga, D- anamjibu majaribio yameahirishwa kwa siku moja. I- anamwambia hiyo ni vizuri zaidi maana watapata muda mwingi wa kujiandaa.

D-503 anaondoka kurudi kwake, njiani anapishana na watu lakini anajiona ni mpweke. Maana hao wote wanakwenda kupata ukombozi, ila yeye hataupata kwa sababu hataki kukombolewa.

👉32

D-503 yuko kazini, anatafakari kama anaamini kuna kifo, anajiambia ndiyo, kila binadamu atakufa. Lakini je yeye anaamini kwamba mwili alionao utakufa na kuoza? Anasema kila mtu hujisahaulisha hilo, ndiyo maana hatujiui, tunailisha na kuivalisha miili yetu.

Mfanyakazi mwenzake anamuuliza ni mafuta kiasi gani watapaswa kuweka kwenye chombo cha angani siku ya majaribio. D-503 anajibu yani 15 zinatoshwa kwa safari ya masaa matatu, lakini bora wakaweka tani elfu moja.

Mwenzake anashangaa, ya nini mafuta mengi hivyo? D- anamjibu huwezi kujua, lolote laweza kutokea. Wakiwa hapo wanaona msafara wa watu wakipita na kuzunguka mitaani. Ni watu ambao wamepatiwa tiba mpya, akili zao zinakuwa kama zimeharibika na hawawezi kufikiri tena kama awali, wanafuata kile wengine wanafanya.

Kila anayewaangalia watu hao anapatwa na hofu kuhusu tiba hiyo mpya.

D- akiwa anaenda nyumbani anakutana na O- ambaye anamwambia hayuko tayari kwa riba hiyo. D- anamwambia ni wakati wa kwenda kwa I- ili awasaidie, anakubali.

Wakiwa wanaongozana, D- anagundua kuna mtu anawafuata nyuma, kuangalia ni S-. Anabadili safari, badala ya kwenda kwa I- anarudi kwake.

O- anamwambia mbona amemdaganya, anamwonesha S- na kumwambia kila mara amekuwa

anamfuata kama anamchunguza, hivyo hataweza kumpeleka kwa I-. Ila anaandika ujumbe na kumpa, anamwambia aende nao kwa I-. Anamuaga na O- anaondoka.

Kwenye jengo analokaa pia kuna watu wamepata tiba mpya na wanaonekana kurukwa na akili, wanaeleza kuona watu wa zamani kwenye nyumba ya kale.

D- anajiuliza kama siyo ambacho yeye amekuwa anaona wakati wote. Anajiambia watu hao hawajarukwa na akili, wanachoeleza ni kweli.

👉33

Siku mpya, D-503 anasoma taarifa muhimu kwenye gazeti ambayo imeandikwa kwa herufi kubwa; MAADUI WA FURAHIA WAMEAMKA, SHIKILIA FURAHIA YAKO KWA MIKONO MIWILI. KESHO KAZI ZOTE ZITASIMAMA NA WATU WOTE WATAPEWA TIBA MPYA, ATAKAYEKATAA ATAPATA ADHABU YA KIFO.

D-503 anakatishwa tamaa na tangazo hilo, anaona huo ndiyo mwisho wake kama anavyojifahamu. Anakiangalia chumba chake ambacho hatakiona tena kama kilivyo.

Anaziweka karatasi za aliyoandika kabatini, akijiambia haina tena matumizi maana hakuna atakachokumbuka.

Anajiambia leo ndiyo siku yake ya mwisho na kesho atakuwa mtu mwingine.

👉34

Ni siku ya kujaribu chombo cha angani. D- na wenzake watatu ndiyo wataendesha chombo. Ndani ya chombo kuna watu wengine na mmoja wao ni I-330 ambaye amepanda kama msaidizi.

D-503 na wenzake wanaweka mpango mzima wa safari, huku yeye pekee akijua nini kitaenda kutokea baadaye, maana atawaacha wote na kuondoka na chombo.

Safari inaanza, chombo kinaondoka kwenye anga la nchi, D- anaita msaidizi mmoja aje kuchukua ujumbe, I- anamfuata. Anaigiza kama anampa maelekezo kwa sauti, huku wakizungumza. I- anamwambia alimpokea O- na ameshamtanguliza. Mpango uendeleo kama walivyoweka, saa sita watu watakapotoka kwa ajili ya kula, wanawafungia nje na kuondoka na chombo.

Saa sita inakaribia, chombo kinatua eneo lenye kijani na watu wanatoka kwa ajili ya kula. Kabla hawajafanya chochote, kwenye chombo anatoka mtu ambaye hawamjui, anamwambia D- wanajua mpango wao wote, na kwa sasa atapaswa kujaribu chombo kama ilivyopangwa na kukirudisha salama Marekani na baada ya hapo hatua dhidi yake zitachukuliwa.

D- anachanganyikiwa kusikia hivyo, anamwambia I- ambaye haonekani kujali kuhusu hilo.

Wanamaliza kula na chombo kinaanza safari ya kurudi.

👉35

Ni siku ya watu kupatiwa tiba mpya. D-503 anatoka chumbani kwake kwenda kwenye meza ambayo U- huwa anakaa lakini hamkuti. Anakumbuka kwa kuwa siku hiyo hakuna kazi, hawezi kuwa hapo.

Anajiambia atamfuata shule ambapo huwa anafundisha watoto, kwenda kwenye kituo cha treni za ardhi, anakuta siku hiyo hakuna huduma.

Anaona watu wakiwa kwenye taharuki kubwa, wapo wanaoenda kwenye tiba na wapo ambao hawataki kwenda.

Mtu anamwambia D- aende kwenye tiba, anasema haitaki tiba hiyo. Mtu huyo anamwambia ni kwa sababu anazitaka tamaa za kijinga, ambazo zitamnyima furaha.

D- anamwambia watu wa kale walikuwa wanaweka karoti mbele ya farasi ili apate tamaa ya kuikimbilia na kwa njia hiyo kuwezesha usafiri. Bila ya tamaa hakuna kinachoweza kufanyika.

Anaamua kurudi nyumbani, akiwa ndani na hajui afanye nini, U- anakuja na kumwambia amesikia kwamba kaumia. Anampa pole na kutaka kumsaidia.

D- anashusha mapazia, U- anakimbilia kwenye mlango ila anamwahi na kuufunga. U- alidhani D- anataka kufanya naye mapenzi, kumbe D- alikuwa anataka kumuua.

Anampiga na chuma na anaanguka chini, D- anabaki akicheka na kuona kicheko ni tiba kubwa. Ghafla simu inaita, anadhani ni I-, anapokea na kusikia sauti inamwambia mimi ni Well-Doer, njoo sasa hivi.

D- anashtuka kwa hilo, anamuangalia U- ambaye amezinduka, anamuuliza kama aliripoti kuhusu I-,

anajibu hapana.

D- anatoka kwenda kwa Well-Doer.

👉36

D-503 anafika kwa Well-Doer, amekaa chini na anamwambia kwa juu, anaona miguu na mikono yake mikubwa, kitu kinachompa hofu sana.

Well-Doer anamwambia na wewe pia, wewe mtengenezaji wa chombo cha angani, ambaye ulipewa nafasi ya juu na jina lako lingeandikwa kwenye vitabu vya historia, umekubali kuwa msaliti?

D-503 hajibu chochote.

Well-Doer anaendelea kumwambia kwamba dunia haijawahi kwenda bila ya watu kutolewa kafara, anamkumbusha mfano wa yesu kuuliwa msalabani. Anamweleza jinsi dini za kale zilivyoamini mungu aliyeua wengi alikuwa mungu wa upendo.

Anamwambia tangu enzi na enzi, watu wanajua kwamba upendo hauji bila maumivu, moto ni mzuri, lakini unaunguza na ukweli huwa unaumiza.

Anamwambia D- kama ana cha kujitetea aseme. D- anafikiria na kuona hana cha kujitetea, maana hizo ni fikra ambazo hata yeye amekuwa nazo kwa muda mrefu ila hakuweza kuzijengea hoja vizuri.

Well-Doer anamwambia kama amekaa kimya maana yake anakubaliana naye, anamtaka waongee kama watu wazima wanavyoongea watoto wakienda kulala.

Anamuuliza kama anakumbuka watu wa zamani walikuwa wanaota kuhusu paradiso, walisubiri kwa hamu siku wakifika paradiso ambapo hawatakuwa na tamaa tena, watakuwa na furaha muda wote.

Anamwambia serikali inachofanya ni kuileta ile paradiso ambayo watu wa kale waliota na kuifanya kuwa uhalisia. Serikali imejua kinachowafanya watu wakose furaha ni tamaa zao na imeweza kuja na njia ya kuondoa kabisa tamaa hizo na maisha yanakuwa furaha kwa asilimia 100.

Well-Doer anaendelea kumwambia pamoja na juhudi zote hizo, bado watu hawaridhiki, bado watu kama yeye D- wanaisaliti serikali.

Well-Doer anamuuliza umri wake, anamjibu miaka 32, anamwuliza kwa nini amekubali kutumiwa kama mtoto wa miaka 16? Anamwambia watu hao walimpenda kwa kuwa ni mtengenezaji wa chombo cha angani na hivyo walimlaghai ili wajipatie chombo hicho.

D-503 anakataa, anasema si kweli, I- alimpenda kweli. Anatoka akikimbia na kusema anatamani amuone kwa mara ya mwisho, kabla ya adhabu yake ya kifo.

👉37

Wako kwenye chakula lakini D-503 hawezi kula, aliyekaa pembeni yake anamwambia wanamuangalia kwa nini hali, hivyo ale.

Wakiwa hapo wanasikia mlipuko mkubwa, ukuta wa mji umevunjwa.

D-503 anatoka akikimbia na kila anayekutana naye anamuuliza kama amemuona I-330, hakuna anayemjibu.

Anaenda mpaka kwenye jengo alilokuwa anakaa I- anaingia kwenye chumba chake na kukuta vitu vimevurugwa.

Anaona vyeti vingi vilivyoandikwa jina lake, anavikusanya vyote na kisha anavitupa.

Anatoka na kurudi nyumbani, anga limebadilika sana tangu ukuta umevunjwa.

Anafika nyumbani na usingizi mzito unamchukua.

👉38

D-503 anashtuka usingizini na kumuona I-330 akiwa amekaa kwenye kiti hapo chumbani kwake.

Anaamka na kumfuata, hajui aseme nini.

Anajikuta anamwambia amemtafuta sana, ameenda kwake hataki kumpoteza.

I-330 anamwambia muda wake ni mchache, wenzake wanamsubiri chini hivyo amekuja kumuaga.

Anashusha mapazia na anamkumbatia na kumbusu.

I-330 anamuuliza amesikia alienda kwa Well-Doer, anamjibu ndiyo na anamsimulia yote waliyoongea, ila hamwambii kwamba alimwambia anampenda kwa kuwa wanataka chombo cha angani.

Wanafanya mapenzi kisha I- anaondoka, D- anabaki akiwa anajisikia vibaya na hana msukumo wa kufanya chochote.

👉39

D-503 anachelewa kuamka, ni saa nne asubuhi, hajaisikia kengele siku hiyo.

Amepanga ajiue, lakini kabla anataka aeleze kila kitu.

Anatoka na kwenda ofisi ya malezi, anakuta watu wengi wanasubiri kuhudumiwa.

Anamuona S- anaingia ofisini kwake. Anamwambia amekuja kukiri yote.

S- anamsikiliza, anaeleza kila kitu tangu siku ya kwanza kukutana na I- tangu alipoanza kujiona na nafsi mbili, vyeti feki vya ugonjwa na mpaka kutoka nje ya ukuta.

S- anamsikiliza kwa makini kisha anamwambia bado kuna kitu anamficha, anamwambia siku aliyotoka nje ya ukuta, hakumuona yeye?

D-503 anataharuki kwa hilo, anaona huenda S- naye ni mmoja wao, anatoka haraka kwenye ofisi yake na kujikuta yuko kwenye choo cha kituo cha treni.

Anapanga kukamilisha lengo lake la kujiua, aliyekuwa upande wa pili wa choo anamwambia anamuelewa kile anachopitia na anapaswa kujua kila kitu kina mwisho, hata dunia na vyote vilivyopo vina mwisho wake.

D-503 anakiri hilo ni kweli, japo watu hawapendi kukubali, lakini yote yalipo yana mwisho na zimabaki hadithi.

Anamuomba mtu huyo karatasi ili amalizie kuandika matukio hayo ya mwisho na kufika mwisho wa maisha yake.

👉40

D-503 pamoja na yule aliyekutana naye chooni na wengine wanakamatwa kwa nguvu na kwenda kupewa tiba mpya.

Baada ya kupata tiba hiyo, D-503 amekuwa na utulivu mkubwa, ile hali ya kuota haipo tena wala hajioni kwa nafsi mbili.

Anaenda tena kwa Well-Doer na kueleza kila kitu bila kuficha chochote.

Kisha mwanamke na watu wengine wanaletwa mbele yake ili wakiri, wanateswa sana, mwanamke hakiri chochote ila wenzake wanakiri.

Siku inayofuata wanaenda kuuawa, ukuta uliovunjwa unarekebishwa.

D-503 anajiambia wamepata ushindi, fikra zimeshinda.

👉SOMO

Hii ni riwaya iliyobeba mambo mengi kuhusu maisha. Japo simulizi yake ni ya miaka mingi ijayo na vingi vinavyoelezwa vinaonekana ni vya kusadikika, kuna mengi ya kujifunza kuhusu maisha kutoka kwenye riwaya hii.

1. Tunajifunza kuhusu udhibiti wa serikali, kila serikali hupenda kudhibiti raia wake na mara nyingi hilo huwa haliendi vizuri. Kwani watu wanapozuiwa kufikiri au kuwa huru , hutafuta kila njia ya kuasi.

2. Tumejifunza kuhusu uhuru na furaha, inaonekana ni vitu ambavyo haviwezi kuwa pamoja. Kwa upande wa utawala, unaweza kuona hivyo, ndiyo maana hata baadhi ya serikali au viongozi huona mfumo wa demokrasia unachelewesha maendeleo. Lakini ukweli ni hata mtu awe na kila anachohitaji, kama hatupo huru hatatulua, hatakuwa na furaha, atatafuta tu namna ya kuasi. Hivyo uhuru na furaha vinapaswa kwenda kwa pamoja, kwa mtu mwenyewe kujua jinsi ya kutumia uhuru wake.

3. Tunajifunza pia jinsi watu wanavyoweza kutulaghai kwa mapenzi kumbe wanataka kututumia kwa manufaa yao binafsi. Hilo lipo sana, kuna watu wanaweza kukuingiza kwenye mtego wa mapenzi, ukawapenda kweli na ukaona wanakupenda, kumbe wanakutumia ili kupata wanachotaka.

Tunapaswa kuwa makini sana kwenye hili.

4. Tumejifunza pia kwamba huwezi kupata bila kupoteza. Baadhi ya vitu kwenye maisha unavipata baada ya kupoteza vitu vingine. Tumeona jaribio la kuwaondolea watu tamaa kabisa, likiwaacha wakiwa hawawezi kufanya maamuzi yoyote. Hapa pia tunajifunza hata madhaifu tuliyonayo, kuna wakati yana msaada mkubwa.

5. Tumejifunza pia kwamba asili ya binadamu huwa haibadiliki. Teknolojia inaweza kuwa kubwa sana, lakini binadamu wanabaki kuwa binadamu. Tumeona jitihada za kutumia teknolojia kuondoa wivu zimeshindwa, bado watu wanapatwa na wivu pale hisia zao zinapokuwa juu.

Muhtasari huu umeandaliwa na Kocha Dr Makirita Amani,

www.t.me/somavitabutanzania